

KILIMO CHA MATIKITI MAJI: MASOKO NA FURSA ZA KIBIASHARA

Mtalula MohamedMtalula Mohamed

March 28, 2023

Karibu kwenye makala hii inayohusu Kilimo cha Matikiti Maji Tanzania. Kama mkulima mzaoefu na mtaalam wa kilimo cha matikiti maji, muda mfupi ujao nitakupa mwongozo wa kitaalam juu ya mbinu bora za uzalishaji, masoko na fursa za kibiashara katika kilimo hiki.

Matikiti maji hulimwa kama zao la biashara katika sehemu nyingi duniani zenye hali ya hewa ya joto la wastani. Zao hili lina wapatia watu shughuri za kufanya na hivyo kuwapatia kipato kuanzia kwenye nyanja za uzalishaji hadi kwenye matumizi.

Matikiti maji ni mojawapo ya jamii aina ya matunda au mbogaboga inayotambaa. Mimea hii inapatikana katika kundi linalojumuisha mimea mingine (curcubitaceae family) kama matango, maboga na maskwash (squash).

Tikiti maji ni zao la kipekee ambalo limekuwa likibamba soko la ndani na nje ya Tanzania kutokana na ladha yake nzuri, faida zake kiafya, na matumizi yake katika viwanda vya chakula na vinywaji. Hata hivyo, ili kuweza kunufaika na soko hili, mkulima anahitaji kujua mbinu bora za kilimo, mahitaji ya soko, na fursa za biashara.

Katika makala hii, nitaelezea kwa kina kuhusu masoko ya matikiti maji Tanzania, mahitaji ya soko, jinsi ya kuongeza uzalishaji, na fursa za biashara. Nitakupa miongozo na mikakati ya kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi, na kujenga uhusiano mzuri na wanunuzi na wazalishaji wa viwandani.

Kupitia makala hii, utajifunza jinsi ya kuongeza uzalishaji wa matikiti maji, jinsi ya kujenga thamani ya matunda yako, na jinsi ya kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, endelea kusoma ili kuweza kujifunza zaidi kuhusu Kilimo cha tikiti Maji Tanzania na fursa zake za biashara.

Uchaguzi wa eneo linalofaa

Matikiti maji husitawi katika maeneo yenye joto la wasitani yaani haihimili hali ya joto kali sana, baridi kali, mvua nyingi wala udongo unaotumisha maji, magonjwa ya fangasi na wadudu waharibifu.

Joto: Matikiti hukua vizuri katika maeneo yenye joto la wastani wa nyuzi kati ya 21 – 30 sentigradi. Iwapo mitikiti itapandwa katika maeneo yenye joto chini ya nyuzi 15 za sentigrade huchelewa kuota.

Mvua: Matikiti maji yanahitaji kiasi cha mvua kati ya millimita 400 – 600 kwa msimu. Mvua nyingi husababisha uwepo wa magonjwa ya fungasi na bakteria ambayo huathili mavuno.

Hali ya Udongo: Kilimo cha matikiti huhitaji udongo wenye rutuba nzuri ulio na virutubisho. Vile vile haihitaji udongo wenye kiasi kikubwa cha tindikali na alikali kubwa. Hali ya udongo katika kipimo cha pH iwe kati ya 6.0 na 7.0. Ingawa mmea una uwezo vile vile wa kuhimili kwenye udongo wenye pH 5.0

Mikoa ya Tanzania: Kilimo cha matikiti maji kinakubali vizuri kwenye ukanda wa pwani na miinuko kidogo kama DSM, Tanga, Morogoro, Mtwara, Lindi na Pwani ambapo kuna jua la kutosha. Muda mzuri wa kupanda ni kipindi cha kipupwe mwezi wa tatu mpaka wa tisa.

Uandaaji wa Shamba

Fyeka vichaka na ng'oa visiki vyote. Katua kwa kina cha sm 22.5 kwenye Sesa. Kabla ya kupandikiza udongo utifuliwe vizuri na majani yaondolewe kabisa. Shamba liandaliwe vizuri kwa kusafisha ili kuondoa mimea mingine ambayo inaweza kuwa ni chanzo cha magonjwa. Weka mbolea ya samadi debe moja kwa kila mita 10 za eneo. Tengeneza matuta katika sehemu ambayo ina majimaji.

Mbegu Bora za Matikiti

Mbegu bora za tikiti maji zipo nyingi sana, zifuatazo ni baadhi tu ya mbegu hizo na makampuni yanayozalishaji mbegu hizo.

Arashani F1 – kutoka Syngenta

Sukari F1 – Kutoka East Africa seeds

Sugar king F1 – kutoka Africasia

Juliana F1 – kutoka Kiboseed

Zebra F1 – Kutoka Balton

Pato F1 – Kutoka Agrichem

Soma hapa mbegu Mpya zilizotangazwa na Kamati ya Taifa ya mbegu

Maamuzi ya mbegu nzuri ya kupanda nashauri yaanzie sokoni. Lijue soko lanko, soko ambalo utauza mazao yako. Jifunze bidhaa wanaipenda, yaani wanapenda matikiti ya aina gani? Ukishajua basi utajua mbegu ya kununua na kupanda. Lakini pia hakikisha hiyo mbegu inakubali katika eneo lako kwani kila mbegu ina maelezo ya maeneo inayofanya vziuri.

Upandaji wa tikiti maji

Katika shamba la ukubwa wa hekta moja kiasi cha kilo 3 – 4 cha mbegu kinaweza kutumika. Panda mbegu 2 au 3 moja kwa moja katika kila shimo. Usipande katika kitalu kwasababu miche ya mitikiti huwa ni dhaifu sana wakati wa upandikizwaji iwapo itapandwa kwenye kitalu hivyo kupelekea kufa kwa miche hiyo. Panda umbali wa sentimeta 2 chini ya udongo kwa umbali wa mita 1 hadi 2 kutoka shina hadi shina na mita 1.5 – 3 kutoka mstari hadi mstari.

Kwenye makala yetu ya kanuni za kilimo bora tumeeleza kwa kina umuhimu wa kuzingatia nafasi za kupandia na athari zake iwapo hutozingatia.

Zingatia: usitumie mbegu za tikiti ulilonunua (kwa ajili ya kula) kwasababu linaweza kuwa ni chotara (Hybrid) ambayo hupelekea kushusha kiasi na ubora wa matikiti yatakayo zaliwa kwa sababu yatakuwa ni kizazi cha pili (F2).

Tuna Mwongozo wa kilimo biashara wa zao hili, kwanini usiupate ili upate maelezo mengi yenye kina zaidi?

Kwenye mwongozo utapata mapendekezo maalum kutoka kwetu juu ya aina bora na kiasi sahihi cha mbegu, mbolea na viuatilifu. Pamoja na uchambuzi wa gharama za uzalishaji katika kila hatua na faida utakayopata.

Kupandikiza na kupunguzaji miche

Mimea ya mitikiti huanza kuota baada ya kama wiki 2 hivi. Inapoanza kuota ifuatilie kwa ukaribu sana ili ubaini maeneo yote yenye kasoro kama vile mbegu ambazo hazijaota kabisa au zilizoota zaidi ya mbili katika kila shimo.

Pandikiza kila sehemu ambapo mbegu hazijaota au imeota moja tu. Na punguza miche kwenye kila shimo mbalo zimeota zaidi ya mbili. Lengo hapa ni kuhaikisha kuwa unakuwa na mimea miwili katika kila shimo, sio zaidi, sio pungufu. Tumeeleza kwa kina umuhimu wa kuzingatia kupandikiza na kupunguzia miche kwenye makala ya kanuni za kilimo bora hapa.

Angalizo: Usinga'oe mche bali ukate ili kuzuia kusumbua mizizi ya mche uliobaki. Vilevile unaweza kupandishia udongo kwenye mashina ili kusaidia kupunguza maji kutuama kwenye mimea yako, pia unaweza kuweka samadi badala ya kupandishia udongo ukiwa na nia ileile ya kuzuia maji yasisitua na kuongeza rutuba.

Umwagiliaji

Shamba linatakiwa limwagiliwe mara kwa mara wakati kiangazi. Kipindi muhimu zaidi ambapo mimea hii huhitaji maji zaidi ni katika kipindi cha uotaji wa mbegu, wakati wa kutoa maua na siku takribani kumi kabla ya kuvuna. Iwapo kutakuwa na ukosefu wa maji kutasababisha kutengenezwa kwa matunda ambayo si mazuri na yenye umbo baya, pia kupungua kwa ukubwa wa matunda.

Mzunguko wa umwagiliaji utategemea mambo yafuatayo: mfumo wako wa umwagiliaji, msimu au hali ya hewa, aina ya udongo wako na hatua ya ukuaji wa zao lako.

Angalizo: usimwagilie matikiti wakati wa jioni sana au usiku kwasababu inaweza kusababisha magonjwa ya majani kutokana na unyevu kukaa muda mrefu. Vile vile usimwagilie juu ya maua wakati wa asubuhi au jioni kwasababu unaweza kuzuia wadudu kama nyuki ambao ni muhimu sana wakati wa uchavushaji.

Mahitaji ya Mbolea ya Matikiti Maji

Mbolea ya kupandia: Wakati wa kupanda tumia DAP weka gram 5 kwa kwa kila shimo (lenye mbegu moja, na weka gram 10 au 15 kama kuna mbegu 2 au 3), hakikisha mbolea na mbegu havigusani.

Mbolea ya kukuzia: Wiki mbili baada ya miche yako kuota weka mbolea ya kiwandani NPK (Yaramila winner) gram 5 tena kwa kila mche, hakikisha unaichimbia chini na isigusane na mmea. Weka mbolea yenye Calcium kama Yaramila nitrabo au CAN gram 10 kwa kila shina unapoona matunda yameanza ili kusaidia kupata matunda makubwa na mazuri.

Kwa ekali 1 ya matikiti utahitaji mfuko mmoja wa DAP, mmoja wa NPK na mmoja wa CAN ikiwa utabakiza miche miwili kwa kila shimo.

Kwa makadirio ya karibu ujazo wa kifuniko kimoja cha maji safi au soda take-away ni sawa na gram 5 hivyo ili upime gram 10 jaza vifuniko viwili vya maji safi. Soma hapa mahitaji ya mbolea katika mahindi

Uwekaji wa matandazo (Mulching)

Matandazo ina maana ya kutumia nyasi na mabaki ya mimea mingine kufunika udongo. Baada ya miche kutambaaa kwa kiasi unaweza kuweka matandazo (mulches) ambayo yaweza kuwa nyasi kavu kwenye udongo ili kuzuia upotevu wa unyevu vile vile kupunguza uotaji wa magugu shambani kwako. Vile vile matandazo yakioza yanaongeza rutuba kwenye udongo na hulinda udongo dhidi ya mmomonyoko wa udongo.

Mkulima akiwa kwenye shamba la matikitiMkulima akiwa kwenye shamba la matikiti

Wadudu na Mgonjwa hatari ya Matikiti maji

Wadudu Waharibifu wa Matikiti Maji

1. Nzi weupe [White flies]

Dalili: Wadudu hawa wanaonekana kama nzi weupe na huwa wanakaa juu ya majani, na hutoa juisi inayoweza kusababisha ukuaji wa kuvu na kuonekana kwa kuvu nyeupe kwenye majani.

Madhara: Huleta madhara kwa kusababisha uharibifu wa majani na kusambaza magonjwa.

Udhibiti: Njia za kuwadhibiti ni pamoja na kutumia mitego yenye feromoni, na kutumia wadudu wanaowala kama vile Entomopathogenic fungi. Dawa za kuwadhibiti ni pamoja na imidacloprid, acetamiprid, na thiamethoxam.

2. Nzi wa matunda [Fruit flies]

Dalili: Wadudu hawa huonekana wakizurura kwenye matunda ya tikiti maji, na pia hutaga mayai yao kwenye matunda yanayoanza kukomaa.

Madhara: Mayai yanayotagwa na nzi wa matunda hupelekea kuwa na matunda yasiyo na ubora na yanayoharibika.

Udhibiti: Njia za kuwadhibiti ni pamoja na kutumia mitego yenye feromoni, kuondoa matunda yaliyooza na kuharibiwa, na kuzingatia usafi wa bustani. Dawa za kuwadhibiti ni pamoja na spinosad, malathion, na deltamethrin.

3. Mende wa matango [Curcubit beetles]

Dalili: Mende hawa huonekana wakizurura kwenye majani na maua ya mimea na na kuyala. Na pia hutaga mayai yao kwenye majani.

Madhara: Wadudu hawa hula majani na maua ya mimea, hivyo kupunguza uzalishaji.

Udhibiti: Njia za kudhibiti wadudu hawa ni pamoja na kutumia mitego ya kuvuta wadudu [feromone hormone], kutumia wadudu wanaowala kama vile *Bacillus thuringiensis*, na kutumia dawa za kudhibiti wadudu kama vile Carbaryl, Malathion, na Imidacloprid.

4. Nzi wa matikiti [Melon flies]

Dalili: Wadudu hawa huonekana wakizurura na kula majani, maua na matunda ya mimea na hutaga mayai yao kwenye matunda yanayokua.

Madhara: Mayai yanayotagwa na nzi hawa hupelekea kuwa na matunda yasiyo na ubora na yanayoharibika.

Udhibiti: Njia za kuwadhibiti ni pamoja na kuondoa mimea iliyoambukizwa na kuweka mitego yenye feromoni. Dawa za kuwadhibiti ni pamoja na carbaryl, malathion, na permethrin.

5. Vidukari [aphids]

Ni wadudu wadogo, wenye miili laini ambao hukusanyika kwenye majani na shina.

Dalili: Wadudu hawa wanaweza kuwa rangi ya kijani, nyeusi, au nyeupe na huwa wanakaa juu ya majani na shina.

Madhara: Wanaweza kusababisha manjano na kujikunja kwa majani, kudumaa kwa ukuaji na kupunguza mavuno. Wanaweza pia kutoa umande ambao huvutia mchwa na ukuaji wa fangasi.

Udhibiti: Nyunyiza kwa maji ya sabuni. Changanya kijiko kikubwa kimoja cha sabuni ya maji kwenye lita 1 ya maji na nyunyiza sehemu zote za majani. Dawa za kuwadhibiti ni pamoja na imidacloprid, acetamiprid, na thiamethoxam.

6. Vithiripi [thrips]

Ni wadudu wembamba wenye mabawa yenye pindo ambao hula maua na matunda.

Dalili: Wadudu hawa ni wadogo sana na huwa wanakaa kwenye majani na maua.

Madhara: Wanaweza kusababisha makovu na kuharibu maumbo ya matunda, kupunguza ubora wake na hatimaye soko lake. Wanaweza pia kusambaza virusi kwa mimea.

Udhibiti: Nyunyiza kwa maji ya sabuni. Changanya kijiko kikubwa kimoja cha sabuni ya maji kwenye lita 1 ya maji na nyunyiza sehemu zote za majani. Dawa za kuwadhibiti ni pamoja na spinosad, acetamiprid, na imidacloprid.

7. Sota [Cutworms]

Dalili: Wadudu hawa ni viwavijeshi ambao hukata mashina ya miche wakati wa usiku na kusababisha mimea kuanguka. Sota huleta madhara makubwa hasa kwa mimea michanga.

Madhara: Uharibifu wa shina unaweza kusababisha kupoteza miche yote, na hivyo kupunguza uzalishaji.

Jinsi ya kudhibiti: Njia za kuwadhibiti ni pamoja na kutumia mitego, kuchimba mashimo karibu na mimea, na kutumia dawa kama Carbaryl, Diazinon, au Chlorpyrifos.

8. Utitiri [Spider mites]

Utitiri ni wadudu wadogo sana ambao hushambulia majani ya mimea na kusababisha majani kuwa ya manjano, na baadaye kubadilika kuwa ya kahawia.

Dalili: Majani ya tikiti maji yanageuka rangi na kuwa manjano kabla ya kupauka na kufa.

Madhara: Utitiri huacha nundu nyeupe kwenye majani ambayo huwa kama ishara ya kuharibika kwa majani na kusababisha upungufu wa juisi ndani ya majani ya tikiti maji. Hii inaweza kusababisha mimea kudumaa, kupoteza majani, na kusababisha uharibifu wa mazao.

Jinsi ya kuwadhibiti: Njia ya kuzuia ni kuhakikisha unahifadhi usafi wa shamba na kuzuia wadudu hawa kuenea. Matumizi ya mimea yenye harufu kama vile lavender, peppermint, na garlic huweza kuwazuia utitiri. Dawa zinazoweza kutumika ni pamoja na sulphur, Neem oil, na Acaricides.

Magonjwa ya Matikiti maji

1. Ukungu jani wa Alternaria [Alternaria Leaf Spot]

Chanzo: Fangasi anayelitwa Alternaria cucumerina.

Dalili: Madoa meupe hadi kahawia yenye umbo la duara kwenye majani ya mimea ya tikiti maji. Madoa haya hukua na kuwa makubwa kadiri yanavyoendelea kuenea na kuharibu majani.

Uharibifu: Ugonjwa huu unasababisha upungufu wa majani kwenye mmea wa tikiti maji, kupungua kwa ubora wa matunda, na kupungua kwa mavuno ya mmea.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa *Alternaria Leaf Spot* ni pamoja na kuepuka kupanda tikiti maji kwenye udongo ulio na mvua nyingi na unyevu mwingi, kuondoa majani yaliyoathiriwa na ugonjwa, na kutumia dawa za kudhibiti magonjwa kama vile Chlorothalonil, Mancozeb, na Azoxystrobin.

2. Ugonjwa wa kutoka utomvu [Gummy Stem Blight]

Chanzo: Fangasi anayelitwa *Didymella bryoniae*.

Dalili: Madoa madoa ya rangi ya njano au hudhurungi yenye umbo la mviringo au mviringo uliochongoka kwenye majani; kutoka utomvu wenye rangi ya hudhurungi au nyeusi kwenye shina na matunda [gummosis]. Ugonjwa huu unaweza kuenea kwa kasi katika hali ya joto, yenye unyevunyevu.

Uharibifu: Kupunguza uwezo wa mmea wa kupumua na kufanya usanisinuru. Ugonjwa huu husababisha mmea kukauka na kufa, na hivyo kupunguza uzalishaji wa mmea wa tikiti maji.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa Gummy Stem Blight ni pamoja na kupanda mimea kwa nafasi inayofaa [mistari iwe umbali wa mita 1.5 hadi 3] na kuzingatia mzunguko wa mazao, kuondoa majani yaliyoathiriwa na ugonjwa, na kunyunyizia dawa za fangasi kama vile Thiophanate-methyl na Carbendazim.

3. Mnyauko fusari [Fusarium Wilt]

Chanzo: Fangasi anayelitwa *Fusarium oxysporum*.

Dalili: Dalili za ugonjwa huu ni majani kuonekana ya manjano, mmea kukauka, na kuoza kwenye shina na mizizi ya mmea. Mnyauko *Fusarium* unaweza kudumu kwenye udongo kwa miaka mingi, na hivyo kufanya kuwa vigumu kudhibiti.

Uharibifu: Kupoteza maji na virutubisho vya mmea; kudhoofisha au kuuu mmea kabisa, hivyo basi kusababisha kupungua kwa ubora na kiasi cha mavuno kwa mazao ya tikiti maji.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa *Fusarium Wilt* ni pamoja na kutumia mbegu bora zisizo na maambukizi; kupanda tikiti maji katika udongo wenye pH ya 6.5-7.0; kutumia mbolea za phosphorus; kupanda tikiti maji katika maeneo mapya yasiyoathiriwa na ugonjwa huo; kunyunyizia dawa za fangasi kama vile copper, benomyl au thiophanate-methyl mara kwa mara.

4. Muozo mkaa [Charcoal Rot]

Chanzo: Fangasi anayelitwa *Macrophomina phaseolina*.

Dalili: Mmea unaonekana kuishiwa nguvu, majani hupoteza rangi yake na kuwa na rangi ya njano, na mizizi ya mmea huonekana kuwa na rangi nyeusi kama mkaa.

Uharibifu: Ugonjwa huu unaweza kusababisha kufa kwa mmea wa tikiti maji na kupunguza mavuno ya mmea.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa Charcoal Rot ni pamoja na kuepuka kupanda tikiti maji kwenye udongo wenye unyevu mwingi, kuhakikisha udongo umekauka kikamilifu kabla ya kupanda, na kutumia dawa za fangasi kama vile Azoxystrobin, Carbendazim, na Flutolanil.

5. Ubwiri unga [Powdery Mildew]

Chanzo: Fangasi wa familia ya Erysiphaceae [*Erysiphe cichoracearum*]. Also *Sphaerotheca fuliginea*.

Dalili: Majani yaliyoshambuliwa huonekana kama yamemwagiwa unga au majivu meupe upande wa juu na unga huu unaweza kusambaa hadi kwenye shina na matunda ya mmea.

Uharibifu: Ugonjwa huu unaweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa mmea wa tikiti maji na kuharibu ubora wa matunda.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa Powderly Mildew ni pamoja na kuepuka umwagiliaji wa maji kwenye majani ya mmea, kupunguza unyevu kwenye mazingira, na kunyunyizia dawa za fangasi kama vile Azoxystrobin, Sulphur, na Potassium Bicarbonate.

6. Ubwiri vinyoya [Downy Mildew]

Chanzo: Fangasi wa familia ya Peronosporaceae [*Peronospora parasitica*]

Dalili: Majani yaliyoshambuliwa hugeuka rangi na kuwa kama ya njano, huku baadhi ya majani yakiwa kama yanakauka na madoadoa meusi kwa mbali. Kwenye sehemu ya chini ya jani huonekana ukungu mweupe au wa rangi ya zambarau ambao huenea haraka na kufunika jani lote. Majani yaliyoathirika sana hugeuka rangi na kuwa kahawia au nyeusi na kuanguka.

Uharibifu: Ugonjwa huu husababisha kupungua kwa usanisinuru (photosynthesis) kutokana na kuharibiwa kwa majani. Hii husababisha kupungua kwa ukuaji wa mimea na matunda. Matunda yaliyoathirika huwa madogo, yasiyoiva vizuri na yenye ladha mbaya.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa Down Mildew ni pamoja na kuepuka umwagiliaji wa maji kwenye majani ya mmea, kupunguza unyevu kwenye mazingira, na kutumia dawa za fangasi kama vile Azoxystrobin, Propineb, na Metalaxyl na Mancozeb.

7. Mnyauko bakteria [Bacteria Wilt]

Chanzo: Bakteria wa aina ya *Erwinia tracheiphila*. Usichanganye na *Ralstonia solanacearum* ambaye husababisha mnyauko bakteria kwenye jamii ya nyanya.

Dalili: Dalili za ugonjwa wa ukungu wa bakteria katika tikiti maji ni majani kunyauka ghafla na mmea mzima kufa bila kuonyesha dalili zozote. Majani yanaweza kuwa na rangi ya njano au hudhurungi na kunyauka haraka, wakati shina na marando ya mmea yanaweza kuwa na rangi nyeusi au hudhurungi. Mara nyingi, shina linaweza kupasuka karibu na ardhi.

Pia ukikata shina la mmea ulioathirika, utomvu mweupe wa krimu hutoka. Utauona kwa urahisi zaidi ukiliweka kwenye bilauri angavu yenye maji.

Uharibifu: Ugonjwa wa ukungu wa bakteria husababisha upotevu mkubwa wa mavuno katika zao la tikiti maji, hasa ikiwa ugonjwa huo unatokea mapema katika msimu wa kupanda. Mimea iliyoambukizwa kawaida hufa ndani ya wiki chache baada ya dalili za ugonjwa kuanza kuonekana, na hii inafanya kuwa vigumu kutibu ugonjwa mara baada ya kuenea.

Udhibiti: Nyunyuzia dawa za bakteria kama vile Streptomycin sulfate, Copper hydroxide, na Bordeaux mixture [mchanganyiko wa copper(II) sulphate (CuSO_4) na chokaa (CaO) unotumika kutibu magonjwa ya bakteria na fangasi].

8. Chule [Anthracnose]

Chanzo: Fangasi wa familia ya Colletotrichum [Colletotrichum orbiculare]

Dalili: Majani, shina na matunda ya mmea kuwa na madoa ya kahawia au meusi. Madoa haya huongezeka ukubwa na kuunganika pamoja na kusababisha jani au matunda kukauka na kuanguka.

Uharibifu: Kupunguza uwezo wa mmea wa kupumua na kufanya usanisinuru; kuharibu muonekano wa matunda na kupunguza ubora wake.

Udhibiti: Njia za kudhibiti ugonjwa wa Anthracnose ni pamoja na kuepuka unyevu mwingi kwenye mazingira, kufanya usafi kwenye shamba la tikiti maji, kutoa mimea michanga katika shamba ili kuepuka maambukizi, na kunyunyizia dawa za fangasi kama vile Chlorothalonil, Azoxystrobin, na Propineb.

Uvunaji wa matikiti maji

Matikiti maji ni miongoni mwa mazao yanayochukua muda mfupi sana kukomaa. Kwa kawaida tikiti maji huwa tayari kwa kuvuna baada ya siku 80 hadi 100 tangu kupanda. Vuna wakati matunda yameiva kabisa, usiwahishe wala kuchelewesha baada ya kufika wakati wake. Wakati wote wa uvunaji umakini unahitajika kutoyajeruhi matunda.

Ekari moja huweza kutoa kati ya tani 15 mpaka tani 35 za matikiti kutegemeana na aina ya mbegu na matunzo shambani. Baada ya kuvuna, matikiti yahifadhiwe katika eneo lenye ubaridi wa nyuzijoto 15 hadi 20 za centigrade. Eneo liwe na unyevua-anga (humidity) kati ya 80 hadi 85%. Mahitaji ya soko la Matikiti Maji Tanzania

Matikiti maji ni zao muhimu katika soko la ndani na nje ya Tanzania. Nchini Tanzania, matikiti maji hutumiwa kama chakula cha moja kwa moja na pia hutumika kama malighafi kwa ajili ya viwanda vya kusindika.

Kwa upande wa soko la nje, matikiti maji ya Tanzania huuzwa katika nchi mbalimbali kama vile Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Afrika Kusini, Ulaya, na Mashariki ya Kati.

Mahitaji ya wateja na wasindikaji wa matikiti yanaongezeka kila siku kutokana na faida zake za kiafya na lishe. Matikiti maji yana virutubisho muhimu kama vile vitamini A, C, na E, pamoja na madini kama vile potasiamu na magnesiamu. Aidha, tikiti husaidia katika kuimarisha mfumo wa kinga ya mwili, kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo na kiharusi, na pia husaidia katika kuzuia kansa.

Mbinu za kuongeza thamani ya matikiti maji kwa ajili ya soko la ndani na nje ya Tanzania zinajumuisha mambo kama vile kusindika matikiti maji na kutengeneza bidhaa nyingine kama vile juisi, siagi, na matunda ya kukaushwa.

Hii itasaidia kuhifadhi matikiti maji kwa muda mrefu na pia kuongeza thamani yake. Mbali na hilo, kuhakikisha ubora wa matikiti maji kwa kuchagua wa aina bora za mbegu, mbinu bora za kilimo, na udhibiti wa magonjwa na wadudu pia ni muhimu katika kufikia mahitaji ya masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

Fursa za kibiashara katika Kilimo cha Matikiti Maji

Kilimo cha matikiti maji nchini Tanzania kina fursa nyingi za biashara kwa wakulima. Hapa nitazungumzia fursa tatu kubwa ambazo ni: Ushirikiano na wasindikaji wa matikiti, Kushiriki

katika masoko ya kimataifa ya matikiti au matunda kwa ujumla wake, na Ujasiriamali wa kuongeza thamani ya matikiti maji kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Fursa ya kwanza: Ushirikiano na wasindikaji wa matikiti na matunda maengine. Hii ni fursa muhimu ya biashara kwa wakulima wa matikiti Tanzania. Wasindikaji hawa hununua matikiti maji kwa wingi kutoka kwa wakulima na kisha kuyasindika kuwa juisi, siagi, matunda ya kukaushwa na bidhaa nyingine za matikiti.

Kwa kushirikiana na wasindikaji hawa, wakulima wanaweza kupata soko la uhakika la matikiti na pia kuongeza thamani ya mazao yao.

Fursa ya pili: Kushiriki katika masoko ya kimataifa ya matikiti au matunda kwa ujumla wake. Hii ni fursa nyingine ya biashara kwa wakulima. Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuzalisha matikiti yenye ubora na kwa kiasi kikubwa. Hivyo, kushiriki katika masoko ya kimataifa ya matunda ni fursa kubwa ya kujiongeza mapato na kuongeza thamani ya zao hili.

Kupitia ushirikiano na wafanyabiashara wa kimataifa, wakulima wanaweza kusafirisha matunda nje ya nchi kwa bei nzuri na pia kujifunza teknolojia na mbinu mpya za kilimo.

Fursa ya tatu: Ujasiriamali wa kuongeza thamani ya matikiti maji kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali. Hii ni fursa nyingine tena ya biashara kwa wakulima wa tikiti nchini Tanzania.

Wakulima wanaweza kutengeneza bidhaa kama vile juisi, siagi, matunda ya kukaushwa na bidhaa nyingine za matikiti maji. Bidhaa hizi zinaweza kuuza kwa bei nzuri katika soko la ndani na nje ya Tanzania.

Kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali za matikiti, wakulima wanaweza kuongeza thamani ya mazao yao na kuboresha mapato yao.

Jinsi ya kufikia masoko ya tikiti maji

Kilimo cha tikiti ni moja ya shughuli za kilimo zinazoweza kuleta faida kubwa kwa wakulima nchini Tanzania. Hata hivyo, ili kufanikiwa katika kilimo hiki, ni muhimu kuzingatia njia bora za kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi. Katika sehemu hii, tutazungumzia jinsi ya kufikia masoko ya matikiti maji Tanzania.

1. Kujenga mahusiano mazuri na wateja wa ndani na nje ya nchi

Uhusiano mzuri na wateja ni jambo muhimu sana katika kufikia masoko ya mazao nchini Tanzania.

Kwa mfano, unaweza kujenga uhusiano mzuri na wasambazaji wakubwa wa matunda kama vile supermarket na maduka makubwa ya vyakula ili kuweza kuuza matikiti yako kwa wingi.

Vilevile, unaweza kuwafikia wateja wako kwa njia ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Instagram, na Twitter. Hii itakuwezesha kuwa karibu na wateja wako na pia kutoa taarifa kuhusu bidhaa zako kwa wateja wako wa ndani na nje ya nchi.

2. Kushiriki katika maonyesho ya kilimo na ya biashara

Kushiriki katika maonyesho ya kilimo na maonesho ya bidhaa ni njia nzuri ya kufikia wateja wengi na pia kujenga uhusiano mzuri na wateja wako. Mfano mzuri ni maonyesho ya kilimo ya Nane

Nane yanayofanyika kila mwaka Agosti 8. Na maonyesho ya biashara ya Saba Saba yanayofanyika kila mwaka Julai 7.

Maonyesho haya yanakutanisha wakulima, wafanyabiashara na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi, na hivyo kuwezesha kujenga mahusiano mazuri ya kibiashara. Kupitia maonyesho haya, unaweza pia kujifunza kuhusu teknolojia mpya na mbinu bora za uzalishaji wa matikiti maji.

3. Matumizi ya teknolojia za masoko

Matumizi ya teknolojia za masoko ni njia nyingine nzuri ya kufikia wateja wako. Kwa mfano, unaweza kutumia barua pepe, ujumbe wa maandishi (SMS) au tovuti ya biashara yako kufikia wateja wako wa ndani na nje ya nchi.

Vilevile, unaweza kutumia mitandao ya kijamii na majukwaa ya biashara kama vile Jumia, Kilimo Mart, na Zoom Tanzania ili kuuza bidhaa zako mtandaoni na kufikia wengi zaidi.

Kwa kuzingatia njia hizi za kufikia masoko, utaweza kuuza ya matikiti yako kwa wingi na pia kufikia wateja wengi zaidi ndani na nje ya nchi. Hivyo, ni muhimu kuzingatia njia bora za kufikia masoko ili uweze kuongeza tija kwenye kilimo chako.

Hitimisho

Katika makala hii, tumegusia mambo kadhaa kuhusu kilimo cha matikiti maji Tanzania, ikiwa ni pamoja na Mbinu bora za uzalishaji, faida zake, mahitaji ya soko, fursa za kibiashara, na jinsi ya kufikia masoko ya matikiti maji.

Kilimo cha matikiti maji ni muhimu kwa sababu ni zao linalolimwa kwa wingi nchini Tanzania na linaweza kutoa fursa nyingi za biashara.

Tunapendekeza wakulima wote wa matikiti na mazao mengine ya mbogamboga na matunda kufuata mbinu bora za kilimo, kushirikiana na wasindikaji na wateja, na kutumia teknolojia za masoko ili kufikia masoko mengi zaidi ndani na nje ya Tanzania.

Kwa kuboresha kilimo cha matikiti maji Tanzania, tunaweza kuzalisha mazao mengi zaidi na kuongeza mapato ya wakulima na taifa kwa ujumla.

Imepakuliwa:- 22/08/2024

Inapatikana:- <https://www.mogriculture.com/2016/10/kilimo-cha-matikiti-maji/>